Kanisa Anglikana lazidi kupasuka ▸2



Serikali yasitisha kununua samani kutoka nje ▸3



Chadema kuandamana Dar ▸8



MWANANCHI

www.mwananchi.co.tz

Bei: TSh. 500 Kenya KSh40 | Ijumaa Juni 4, 2010 | Kesho | ISSN 0856-7573 Na 03639

Operesheni kata umeme yaibua mambo mazito

Exuper Kachenje

OPERESHENI kata umeme iliyoanza kutekelezwa na Shirika la Umeme nchini (Tanesco), jana iliibua vituko na siri nzito, huku baadhi ya watu wakijifungia ndani na bihi kizee akiwapigia magoti watendaji wa Tanesco kuwasihi wasimkatie umeme.

Nyumba ya mmoja wa makamanda wa polisi mkoa ni miongoni mwa nyumba zilizokatiwa umeme kutokana na kuwa deni kubwa la mamilioni ya shilingi.

Maajabu yanayofichuka ni pamoja na baadhi ya madeni ya wadaiwa kutoonekana katika kompyuta za wahasibu wa shirika hilo, huku kiongozi wa zoezi hilo Mhandisi wa kudhibiti Mapato wa Tanesco, Mposheleye Mwasenga akiweka bayana kuwa watakaothibitika kuhusika na tukio hilo watapoteza kazi.

Jana timu ya Tanesco ikioongozana na waandishi wa habari iliendesha zoezi hilo katika makazi ya watu jijini Dar es Salaam na kukuta baadhi ya wakazi wakidaiwa hadi Sh19 milioni, wengine wakijiunganishia huduma hiyo kinyemela, hata baada ya kukatiwa.

"Kama akaunti haionekani lazima mtu afukuzwe kazi, tulifanya zoezi la kukata umeme Februari mwaka huu mwenyewe nikiwepo, tukakuta anadaiwa Sh19 milioni leo amejiunganishia umeme, pia tunaambiwa haria deni wakati nina hakika hajalipa, tunakata umeme," alisema Mwasenga.

"Tunamshauri aje alipe. Kama aliunganishiwa na mtu wa Tanesco naye ni kishoka atafukuzwa kazi", alisema Mwasenga katika nyumba namba UK/MMD/265 Ukonga, inayodaiwa kuwa ni ya Clement Mganda anayesadikika kuwa ni mchungaji wa kanisa la "The Winners Chapel" la Ukonga Banana yenye deni la Sh19 milioni.

Katika tukio jingine kwenye operesheni ▸▸4

Uhakiki wa CCJ Dar vurugu tupu

TENDWA ADAI WANACHAMA HALALI NI 13 TU, ZOEZI LASITISHWA

▸▸Habari kamili 4



Mwenyekiti wa CCJ, Richard Kiyabo akizuiwa na mlinzi wake wakati akielekea kwenye meza ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, John Tendwa kumlalamikia kuhusu uhakiki wanachama wa chama hicho viwanja vya Mwembe Yanga, wilayani Temeke, jijini Dar es Salaam jana. Picha na Silvan Kiwale

Sweden yaibana zaidi Tanzania

Wandishi Wetu

BALOZI wa Sweden aliyeitwa nalizamuda wake, Staffan Herzstrom jana alitoa hotuba kali ya kutaka serikali kutekeleza ahadi inazozitoa, ikiwemo kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wote wa kesi kubwa za rushwa na kuondokana na utamaduni wa kulipana posho.

"(Serikali) isiache hata jiwe moja juu ya jiwe jingine," ameeleza balozi huyo katika hotuba yake iliyokuwa na ujumbe mzito kwa serikali wakati wa hafla ya maadhimisho ya siku ya Sweden ambayo ilitumiwa kumuaga.

Katika hotuba hiyo kali inayosisitiza msimamo wa Sweden katika vita dhidi ya rushwa, Balozi Herrstrom alitaja mambo mawili makubwa na muhimu katika kuondoa umaskini ambayo yanatakiwa kushughulikiwa kuwa ni utekelezaji wa maamuzi yaliyokwishafikiwa na sera pamoja na haki za watoto.

Hotuba yake imekuja zaidi ya wiki moja baada ya Sweden na nchi nyingine wahisani kutangaza kuzuia theluthi moja ya mchango wao kwenye bajeti kuu ya serikali ya Tanzania, kufuatia kutoridhishwa na kasi ya utekelezaji wa masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na kubadilisha mfumo wa usimamizi wa fedha za umma na utekelezaji wa mazimio yaliyofikiwa wakati wa kusaini makubaliano ya kutoa fedha hizo.

Nchi hizo zilitangaza kuwa zimezuia Sh297 bilioni kwenye bajeti kuu ya serikali ya mwaka 2010/11 na kwamba, zinaendelea na mazungumzo na serikali, huku zikisema kuwa iwapo serikali haitatekeleza ahadi zake fedha hizo ambazo ni za walipa kodi wa nchi hizo zitahamishiwa kwa asasi zisizo za kiserikali ili ziendelee kusaidia katika kupunguza umaskini.

Jana Balozi Herrtsron, ambaye nchi yake inachangia dola 45 milioni za Marekani kwenye bajeti hiyo, alikuwa mkali zaidi.

"Tekelezeni nia iliyoelezwa ya kushughu- ▸▸4